

**Ripoti ya Mafunzo ya Kuzijua sheria na kanuni za usalama barabarani kwa
wapanda baisikeli Mbondole Secondary School
27-28 Agosti 2009**

Walimu wafuatao ndio walioshiriki kutoa mafunzo: Paulo Hatibu, Mohammed Samweli, Filbert Mbecha, Hamadi Bwaja, Sosthenes Amlima, Hussein Hamza.

Mafunzo yaliendeshwa kwa muda wa siku mbili, yaliyojumisha jumla ya wanafunzi sitini na tano (65). Kati ya hao wanafunzi wawili ni walimu wa shule hiyo Mwalimu Alex na Pazi T.J. na pia kilikuwa na raia mmoja ambaye alipenda kushirik mafunzo. Washiliki wote waliweza kufuzu mafunzo vizuri kwa siku zote mbili tarehe 27/08/09 na tarehe 28/08/07 na kutunukiwa vyeti vya mahudhurio na vifaa vya mavazi ya usalama wakati wanapo endesha baisikeli ikiwemo helmet (kofia) reflective jackets, pia shiriki wa mafunzo wote waliweza kupata huduma ya chakula kwa siku zote mbili. Wanafunzi walikuwa ni waelewa kwani walikuwa watulivu, na kuweza kutusikiliza kwa umakini na wameweza kuyaelewa vizuri masomo yetu. Kwa sababu walikuwa kwelengo la kutaka kujua, ni ilikuwa changamoto kwetu.

Wanafunzi wote walioshiriki mafunzo walikuwa katika darasa moja kutoka na shule kuwa na uhaba wa madarasa na madawati kwa hiyo ilitulazimu kutuma darasa moja na walimu tuligawana vipengele vya kufundisha kama ifuatavyo.

Mwalimu Filbert Mbecha alifundisha malengo matano ya UWABA kwa miaka mitano ijayo kuanzia mwaka 2008 hadi 2012.

Mwalimu Hussein Hamza alifundisha sehemu za baisikeli na kazi zake.

Mwalimu Paulo Hatibu alifundisha jinsi ya kuvaa helmet kwa usahihi.

Mwalimu Sosthenes Amlima alifundisha kucheki baisikeli yako kabla ya kuondoka.

Mwalimu Hamadi Bwaja alifundisha jinsi ya kupanda baisikeli yako na kuanza safari kwa usalama na kudhibiti baisikeli yako.

Mwalimu Mohammed Samweli alifundisha upade ambao unatakiwa kuendesha baisikeli uwapo barabarani.

Na masomo yaliyobaki tulijigawa wawili wawili ili kuonesha ushirikiano. Na kwa upande wa mafunzo ya vitendo tulishirikiana wote.

Nidhamu, walimu wote tuliweza kuwa na ushirikiano sana na nidhamu ya kutosha kati yetu na kwa wanafunzo walimu tulionesha kuwa karibu na wanafunzi na tulipata ushirikiana na walimu wa shule hiyo.

Mgeni rasmi Ndugu Kassimu Yusufu Mng'ombe Diwani wa Kata ya Msongora ndiye aliyekuwa mgeni wetu wa siku ya mwisho wa mafunzo na ndiye aliye watunuki vyeti vya mahudhurio wanafunzi wote walioshiriki na kuwagawia mavazi ya baisikeli, ikiwemo helmet na reflective jacket.

Hotuba ya mgeni rasmi (diwani)

Hotua ya mgeni ilifuata baada ya kupata maelezo ya mkuu wa msafara ya kumkaribisha na kumpa ufafanuzi kuhusu UWABA, mwaka ulioanzishwa UWABA, malengo yetu UWABA kwa miaka mitano ijayo na kazi zetu.

Diwani alianza kutoa shukrani kwetu UWABA na kupitia maelezo aliyopata alisema amefurahi sana kuona UWABA tumeenda sawa sawa na ilani ya chama cha mapinduzi kwa sababu UWABA imeanzishwa mwaka mmoja ina 2006 na shule ya secondary Mbondole hii ni ilani ya CCM ya 2005 ilihaidi kujenga mashule na ndohiyo ambayo UWABA loe wamekuja kufundisha na amesema Diwani Lupilya ndiyo aliyemshauri aweze kutuhitaji kwa sababu shule za kata yake walio wengi wanatumia baisikeli, itakuwa vizuri kama UWABA tutakwenda kuwafundisha juu ya kujua sheria za barabarani, kwa wapanda baisikeli. Lakini kabla ya yeye haja chukua hatua kumbe sisi UWABA tumeshaenda nah ii nikutokana na wanafunzi wengi kutumia baisikeli kuliko shule zilizokaribu na mji. Amesema ni changamoto kwake na anaamini amepata walimu ambao watawafundisha wengine kabla yetu kwa kumshauri mkuu wa shule hiyo.

Pia ameeleza faidi za baisikeli ikiwemo afya, uchumi, usafiri wa haraka, huondoa magonjwa kama presha, kisukari nk.

Changamoto tuliyopata walimu

- Tumeona kupitia mafunzo haya, ni muhimu kuandaa risara ambayo tutakuwa tuna mkabizi mgeni rasmi, ambayo itakuwa inaeleza nini UWABA na malengo yake na kazi zake.
- Tumeona muhimu kuanda zawadi kuwa mgeni rasmi kama helmet na reflective jacket na kwa mkuu wa shule kama kuleta hamasa kwa wanafunzi na jamii.
- Ni muhimu kuwa na zawadi za ziada kwa shule tunazo kwenda kufundisha kutokana na baadhi yao kujitokeza na kutaka kushiriki.

Hii ripoti imeandaliwa na walimu wote walioshiriki utoaji mafunzo Mbondole Secondary School.